Polisi wapambana na madereva Bajaj, watano mbaroni

"Dereva bajaj alikuwa akitamka maneno haya: 'Leo nitakufanyia kitu mmezoea kutukamata kila siku,' baada ya bajaj kuanguka madereva wengine walianza kumshambulia polisi alipozidiwa aliomba msaada na gari ya doria ilienda kuzungumza nao lakini hakukuwa na mwafaka, badala yake waliendelea kurusha mawe na kuchoma matairi barabarani."

Bwire

Berdina Majinge, Mwananchi
bmajinge@mwananchi.co.tz

Iringa. Watu watano wanashikiliwa kwa tuhuma za kushinikiza vurugu kati ya polisi wa doria maarufu Tigo na waendesha bajaj, hali iliyosababisha polisi kuwatawanya kwa kutumia mabomu ya machozi.

Kamanda wa polisi mkoani Iringa, Juma Bwire alisema tukio hilo lilitokea jana saa 5:15 asubuhi baada ya polisi kumkamata mwendesha bajaj akiwa amezidisha abiria na kupakia kinyume na sheria ya usalama barabarani.

Bwire alisema polisi hao wakiwa katika operesheni maalumu ya kukusanya madeni waliona bajaj hiyo na kuikamata ili kuipeleka kituoni. Askari mmoja aliingia katika bajaj hiyo ili kuelekea kituoni.

Alisema baada ya dereva huyo kukamatwa aliongozana na polisi mmoja wakiwa njiani alipindua bajaj ikaanguka, lengo likiwa kumpeleka kwenye kijiwe chake kuhamasisha wenzake kumzuia kufanya kazi yake.

Bwire alisema baada ya kuona hakuna mwafaka gari jingine la doria lilienda na madereva bajaj walilivunja kioo, ikawalazimu Polisi wa Kutuliza Ghasia (FFU) kutumia mabomu ya machozi.

"Mpaka sasa hali ni shwari ingawa kwa taarifa za kiintelijensia zinaeleza walikusudia kuchoma gari la polisi," alisema Bwire.

Mmoja wa waendesha bajaj ambaye hakutaka kutajwa, alieleza kuwa wakiwa kijiwe cha Frelimo waliona babaj inayumba kisha kuanguka na kuona polisi na dereva wakitoka, lakini muda mfupi walitokea askari wengine wakamshambulia dereva.

UWAJIBIKAJI

Makandarasi waonywa, watishiwa kufukuzwa

Bakari Kiango, Mwananchi
bkiango@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda amewaonya na kuwapa siku tano makandarasi wanaosuasua kubadilika kwa kutekeleza majukumu yao akitishia kuwafukuza.

Makonda alieleza hayo jana akisisitiza wasipobadilika atawafukuza na kuwakamata makandarasi wote bila kujali kigezo cha mkataba husika.

"Huwezi kuwa mkandarasi ambaye umesaini mkataba zaidi ya miezi mitatu na ulionyesha uwezo wako kifedha kwenye nyaraka halafu kazi huanzi.Unapiga danadana kwenye kazi na kuleta kero kubwa na kutukwamisha katika kasi tunayoitaka kwa sababu ya uongo ulioonyesha kwenye nyaraka," alisema Makonda na kuongeza:

"Nimebaini baadhi ya makandarasi hata vifaa hawana, hata fedha walizoonyesha kwenye nyaraka hawana huku miradi ikisuasua. Hata wakipewa fedha kidogo za maandalizi wanakwenda kufidia miradi mingine."

Makonda alitumia nafasi hiyo, kuzionya bodi zote za ugavi za mkoa huo zinazotoa zabuni kwa makandarasi wasiokuwa na uwezo, akisema atazifukuza kwenye nafasi hizo.

Wakati huohuo, Makonda ameunda kamati ya wajumbe 14 kuchangisha fedha zitakazotumika kutibu watoto zaidi ya 500 wenye matatizo ya moyo waliolazwa katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Alisema kamati itakuwa na jukumu la kutafuta si chini ya Sh1 bilioni zitakazopelekwa katika taasisi hiyo kwa matibabu ya watoto hao sambamba na kuwakatia bima ya afya.

"Ndugu zangu naomba muwapokee, wenye kampuni, mashirika, taasisi, vituo vya mafuta na mwananchi. Kamati hii itakuja na utaratibu mzuri utakaomwezesha kila mwananchi kushiriki," alisema.

Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda akizungumza na wanahabari ofisini kwake jana, kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo. **Picha na Bakari Kiango**

WAJUE

Makandarasi wanaosuasua wametajwa kuwa ni wanaotekeleza mradi wa uboreshaji mto Ng'ombe, barabara ya Kivule, mito ya Buguruni Visiwani na Tabata na kwenye masoko mbalimbali ambao wamefikisha miezi mitatu tangu wakabidhiwe miradi lakini hawajafanya kazi.

KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA
ILIYOPO DAR ES SALAAM

MAOMBI YA MAREJEO NO. 11/2018

EXIM BANK (T) LTD .... MLETA MAOMBI

DHIDI YA

1. JOHN HARALD CHRISTER ABRAHSSO ... MJIBU MAOMBI WA KWANZA
2. DASCAR LIMITED .... MJIBU MAOMBI WA PILI
3. MAS AND ASSOCIATES COMPANY LIMITED AND COURT BROKER .... MJIBU MAOMBI WA TATU
4. YUSUPH SHABAN MATIMBWA .... MJIBU MAOMBI WA NNE

KWA: (1) DASCAR LIMITED
S.L.P 106160
DAR ES SALAAM

(2) MAS AND ASSOCIATES CO. LIMITED
AND COURT BROKERS,
KASABA STREET
KINONDONI MANYANYA KAWAWA ROAD,
S.L.P 15694,
DAR ES SALAAM

Hii ni kukujulisha kwamba maombi ya marejeo yaliyofunguliwa na muombaji aliyetajwa hapo juu, yamepangwa kusikilizwa katika Mahakama hii tarehe 6 Novemba, 2019 saa 3:00 Asubuhi. Unatakiwa kuhudhuria Mahakamani bila kukosa.

Kama hutahudhuria wewe mwenyewe au Wakili wako, au mtu yeyote kwa niaba yako anayekubalika kwa Mujibu wa Sheria, maombi haya yatasikilizwa na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa amri yangu na kupigwa chapa ya Mahakama hii leo tarehe 21 Oktoba, 2019.

E.F. FUSSI
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI

BILO STAR DEBT COLLECTOR CO. LTD

WE ARE DEALING WITH DEBT COLLECTION AND PROPERTY AUCTIONS
(MABINGWA WA KUKUSANYA MADENI SUGU)
NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) YA KULIPA DENI KWA WADAIWA SUGU.

Sisi Bilo Star Debt Collector Co. Ltd kwa niaba ya mteja wetu na idhini tuliyopewa na mteja wetu **MUHOJI GENERAL SUPPLIES LIMITED**, tumeelekezwa kuwataarifu wadaiwa sugu kuwa mnatakiwa kulipa madeni mnayodaiwa na mteja wetu kwa kipindi kirefu. Wadaiwa sugu ni kama wafuatao:-

Na.	JINA LA MDAIWA
1.	THABIT S. LUNDENGA
2.	MOHAMED MASSOUD
3.	BETTY REMIGIUS
4.	GIDEON MAGUBO/GRADICE. MAGUBO
5.	ZAKARIA M. MASIAGA
6.	MACHERA CHACHA SORONGAI
7.	SCHOLASTICA JAMES MOTTE

Kwamba mnatakiwa kulipa madeni hayo ndani ya siku kumi na nne (14). Pia tumeelekezwa kuwa ikiwa mtashindwa kulipa madeni hayo ndani ya siku kumi na nne (14), tutakamata mali zenu na kuziuza kwa njia ya mnada wa hadhara kufidia kiasi cha madeni mnayodaiwa na mteja wetu.

KWA MAELEZO ZAIDI
Fika ofisi zetu zilizopo Mbezi beach au wasiliana nasi kwa simu namba, 0716 943424, 0719206984,
Email: Bilostarcompany@gmail.com

Mkufunzi aigaragaza tena Udom kortini

James Magai, Mwananchi
jmagai@mwananchi.co.tz

Dar. Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam imethibitisha uamuzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Kanda ya Dodoma iliyokiamuru Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), kumrejesha kazini mkufunzi wake, Iddy Mwerangi ambaye kilisitisha ajira yake tangu mwaka 2011 isivyo halali.

Uamuzi huo ulitolewa na Jaji George Masaju baada ya kutupilia mbali maombi ya marejeo ya Udom kupinga uamuzi wa CMA, wa kumrejesha mkufunzi huyo katika ajira yake.

Katika uamuzi huo ambao *Mwananchi* limeuona nakala yake, Jaji Masaju alikubaliana na hoja za Mwerangi na kuthibitisha uamuzi wa CMA kwamba ni sahihi kwa kuwa imeridhika kuwa aliondolewa katika ajira isivyo halali.

"Kusitishwa kwa ajira yake kwa hakika kulikuwa ni batili kwa kutokuzingatia usawa na haki ya kusikilizwa, hivyo alisitishiwa ajira isivyo haki," alisema Jaji Masaju.

Alisema kwa hali hiyo tuzo ya kumrejesha mjibu maombi (Mwerangi) katika ajira tangu tarehe ya kusitishwa kwa ajira yake, bila kupoteza haki zake zote kwa kipindi ambacho hakuwapo kazini kutokana na kuondolewa isivyo haki, inastahili kisheria. "Kwa kusema hivyo, maombi haya yasiyo na ustahilifu, yanaondolewa," alisema Jaji Masaju.

Chuo hicho kilisitisha ajira ya Mwerangi Desemba 14, 2011 kwa madai ya kushindwa kuendelea na masomo ya Shahada ya Uzamivu ambayo kilidai kumdhamini kwa lengo la kujiendeleza.

Hata hivyo, Mwerangi alifungua malalamiko yake CMA akidai kuwa aliondolewa katika ajira isivyo haki.

Katika uamuzi wake Agosti 12, 2015 CMA ilikubaliana na malalamiko na ushahidi.